TANGAZO LA SERIKALI Na. 711 la Tarehe 28/8/2020

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SURA YA 407

TAFSIRI YA LUGHA YA KISWAHILI

SHERIA YA HUDUMA NDOGO YA FEDHA

[SHERIA KUU]

Toleo hili la Tafsiri kwa Lugha ya Kiswahili la Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha, Sura ya 407 limefanyiwa urekebu kwa mujibu wa Sheria ya Urekebu, Sura ya 4 na kisha kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili, na limechapishwa kwa mujibu wa mamlaka ya kifungu cha 84(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Dodoma,
……………., 2020

ADELARDUS L. KILANGI
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

SURA YA 407

SHERIA YA HUDUMA NDOGO YA FEDHA

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

4. Biashara ya huduma ndogo za fedha.
5. Aina za watoa huduma ndogo za fedha.
6. Sehemu ya biashara.
7. Uendeshaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha.
8. Uwajibikaji wa watoa huduma ndogo za fedha.
9. Kiwango cha chini cha mtaji.
10. Kiwango cha chini cha mali zinazobadilishi-ka kirahisi kuwa fedha taslim.
11. Kuhama madaraja kwa watoa huduma ndogo za fedha.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YANAYOHUSU MASUALA YA UTAWALA

12. Majukumu ya Benki.
13. Mamlaka ya Benki.
14. Kukasimisha mamlaka na majukumu ya Benki.
15. Jukumu la Waziri.

SEHEMU YA NNE
UTOAJI LESENI KWA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA WA DARAJA LA 2 NA 3

16. Katazo la kutoa huduma ndogo za fedha bila leseni.
17. Maombi ya leseni kwa Daraja la 2.
18. Maombi ya leseni kwa Daraja la 3.
19. Utoaji wa leseni kwa mtoa huduma ndogo za fedha wa kigeni.
20. Upitiaji wa maombi.
21. Utoaji leseni.
22. Uhalali wa leseni.
23. Kukataa maombi ya leseni.
24. Maombi mapya na kukata rufaa.
25. Ufutaji wa leseni.
26. Utaratibu wa kufuta leseni.
27. Matokeo ya kufuta leseni.

SEHEMU YA TANO
USAJILI WA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA WA DARAJA LA 4

28. Usajili wa watoa huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 4.
29. Kukataa maombi ya usajili kwa Daraja la 4.
30. Hati ya usajili.
31. Matokeo ya usajili.
32. Ufutaji hati ya usajili.
33. Uendelezaji na uwezeshaji watoa huduma ndogo za fedha.

SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI NA UDHIBITI WA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

(a) Usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha

34. Usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha.
35. Usimamizi na utwaaji.
36. Shughuli zinazozuiliwa na zinazokubalika.
37. Ulipaji wa gawio au riba.
38. Vitabu vya mahesabu na kumbukumbu nyinginezo.
39. Uandaaji wa mahesabu.
40. Ukaguzi wa mahesabu.

41. Uteuzi wa mkaguzi wa ndani.
42. Utoaji wa taarifa za fedha.
43. Utoaji wa taarifa za mikopo.

(b) Usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha

44. Uwasilishaji wa taarifa.
45. Upatikanaji wa taarifa za muda.
46. Usiri.
47. Ukaguzi wa biashara ya huduma ndogo za fedha.
48. Usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha kwa Daraja la 4.
49. Uzingatiaji wa Sura ya 423.

SEHEMU YA SABA
ULINZI WA WATUMIAJI WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

50. Misingi ya kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha.
51. Ukusanyaji wa madeni na fidia.

SEHEMU YA NANE
MAKOSA NA ADHABU

52. Adhabu ya ujumla.
53. Ufililishaji wa makosa.

SURA YA TISA
MASHARTI YA JUMLA

54. Daftari la watoa huduma ndogo za fedha.
55. Utangazaji wa watoa huduma ndogo za fedha.
56. Kinga kwa matendo yaliyofanywa au kutekelezwa kwa nia njema.
57. Masharti ya mpito.
58. Ushirikishwaji wa wazawa.
59. Dhima kwa matendo ya vikundi vya watu.
60. Kanuni
61. Kutotumika kwa baadhi ya masharti kwa Daraja la 4.

SURA YA KUMI
MAREKEBISHO YATOKANAYO

62.-68. Vifungu vimeondolewa.

SURA YA 407

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Sheria ya kuweka masharti ya utoaji leseni, udhibiti na usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha na mambo yanayohusiana na hayo.

1 Novemba, 2019
[T.S. 784 la mwaka 2019]

Sheria Na.
10 ya mwaka, 2018

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina la Sheria

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

3.-Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Benki" maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania;

Sura 342

"benki" maana yake ni kama ilivyo kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha;

"vikundi vya kifedha vya kijamii" maana yake ni kikundi kilichoundwa kwa pamoja na kusimamiwa na wanachama wenyewe na kusajiliwa chini ya Sheria hii kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha ikijumuisha ukusanyaji wa amana kutoka kwa wanachama wake na utoaji mikopo kwa wanachama wake lakini haijumuishi:

(a) vikundi vya kijamii vya kusaidiana vilivyoundwa kwa madhumuni ya kinga na ustawi wa jamii na kiuchumi wa wanachama wake ambavyo havipokei amana na havitoi mikopo kwa wanachama wake kwa kufanya shughuli za biashara ya huduma ndogo za fedha;

(b) vikundi vya watu wenye maslahi maalum, vilabu na vyama vinavyokusanya michango ya fedha kutoka kwa wanachama wake au vinavyopokea misaada ya hisani vilivyoundwa na kusajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Hiari kwa madhumuni ya kuimarisha hali za kiuchumi kwa wanachama wake lakini havifanyi biashara ya huduma ndogo za fedha; na

(c) vikundi vya muda mfupi vinavyoundwa kwa madhumuni ya kupokea michango au upokeaji wa fedha kwa shughuli za kidini au matukio ya kijamii ikijumuisha ndoa au shughuli za familia za kimila zinazofanywa na watu au vikundi;

Sura ya 212

"kampuni inayotoa mikopo" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni na yenye leseni ya kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha;

"Chombo cha ubadilishanaji wa taarifa za mikopo" maana yake ni taasisi maalumu kwa ajili ya kukusanya na kuuza taarifa za wakopaji binafsi na makampuni;

Sura. 211

"Tume " maana yake ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Ushirika;

"Mlaji"maana yake ni mteja au mwanachama wa taasisi inayotoa huduma ndogo za fedha ambaye anajipatia au ana lengo la kujipatia huduma zitolewazo na taasisi ya huduma ndogo za fedha;

"Mamlaka Kasimishwa" maana yake ni taasisi ya umma iliyokasimishwa mamlaka na Benki Kuu ya Tanzania kutekeleza majukumu na mamlaka ya Benki Kuu chini ya sheria hii;

"taasisi" maana yake ni shirika, ubia, udhamini, chama, wanahisa, ushirikiano wa pamoja wa mitaji, ushirika, umiliki binafsi, kikundi au aina nyingine yoyote ya taasisi ambayo haijaorodheshwa katika tafsiri hii lakini inatambulika kama taasisi ikiwa ni pamoja na

Serikali au wakala wa Serikali au taasisi za Serikali;

"mtoa huduma ndogo za fedha wa kigeni" maana yake ni mtoa huduma ndogo za fedha aliyesajiliwa Tanzania ambaye wamiliki wake wengi au wanahisa wake wengi ni wageni;

"taasisi ya fedha" maana yake ni taasisi iliyosajiliwa chini ya sheria husika ambayo ina leseni ya kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria hii;

"biashara ya huduma ndogo za fedha" maana yake ni biashara ya huduma ndogo za fedha inayohusisha kupokea na kutokupokea amana na inajumuisha shughuli ambazo zimeainishwa katika kifungu cha 4;

"mkopo mdogo wa karadha" maana yake ni mkopo unaotolewa kwa njia ya vifaa ambavyo wastani wa thamani yake hauzidi shillingi milioni kumi na muda wa kurejesha mkopo usiozidi miezi 24;

"mkopo mdogo" maana yake ni mkopo unaotolewa kwa biashara ndogo, kaya na watu binafsi kama itavyoainishwa katika kanuni;

Sura. 394 "huduma ndogo za bima" ina maana iliyotolewa katika Sheria ya Bima;

"watoa huduma ndogo za fedha" maana yake ni taasisi au mtu ambaye amesajiliwa au amepewa leseni ya kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Sheria hii ikijumuisha watoa huduma ndogo za fedha wanaochukua na wasiochukua amana kama walivyoainishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha;

Sura. 423 "utakasishaji fedha haramu" ina maana iliyotolewa katika Sheria ya Utakasishaji wa Fedha Haramu;

"sehemu ya biashara" maana yake ni tawi, ofisi, wakala au ofisi inayohamishika ya mtoa huduma ndogo za fedha inayotoa huduma kwa umma;

"Rejesta" maana yake ni rejesta ya watoa huduma ndogo za fedha ilivyorejewa katika kifungu cha 54 cha Sheria hii;

Sura. 211

"SACCOS" maana iliyotafsiriwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika.

SEHEMU YA PILI
WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Biashara ya huduma ndogo za fedha

4.-(1) Biashara ya huduma ndogo za fedha itafanywa na taasisi za huduma ndogo za fedha ambazo:

(a) zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria zao husika na zinazotambulika chini ya Sheria hii; na
(b) zimeanzishwa na kutambuliwa chini ya Sheria hii.

(2) Taasisi za huduma ndogo za fedha chini ya kifungu kidogo cha (1) zitafanya biashara ya huduma ndogo ya fedha kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(3) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (2), biashara ya huduma ndogo za fedha zitakazofanywa chini ya Sheria hii zitajumuisha-

(a) kupokea fedha, kwa njia ya amana au riba inayotokana na amana au mikopo na ambayo inakopeshwa kwa wanachama au wateja;
(b) kupokea akiba na kutoa mikopo au huduma nyingine za kukopesha kwa wajasiriamali wadogo na kaya za kipato cha chini au watu binafsi;
(c) kutoa mikopo midogo, akiba, bima ndogo, mikopo midogo ya karadha, pensheni ndogo na mikopo midogo ya nyumba;
(d) huduma za kuhawilisha na malipo ya fedha ikijumuisha huduma ndogo za fedha kwa njia ya mtandao;
(e) ufanyaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha za bidhaa ikijumuisha utoaji wa mikopo ya bidhaa;
(f) kutoa huduma ya elimu ya fedha; na

(g) huduma nyingine zinazofanana na hizo kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Aina za watoa huduma ndogo za fedha

5.-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, kutakuwa na madaraja manne ya watoa huduma ndogo za fedha kama ifuatavyo:-

(a) Daraja la 1, litajumuisha taasisi za huduma ndogo za fedha zinazochukua amana;

(b) Daraja la 2 litajumuisha taasisi za huduma ndogo za fedha zisizochukua amana kama vile kampuni na wakopeshaji binafsi wanaotoa mikopo ya fedha;

(c) Daraja la 3, litajumuisha Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOs); na

(d) Daraja la 4, litajumuisha vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha;

(2) Taasisi za huduma ndogo za fedha zinazopokea amana chini ya kifungu cha (1)(a) zitasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za fedha.

Sura 342

Sehemu ya biashara

6.-(1) Kila mtoa huduma ndogo za fedha atapaswa kuwa na sehemu ya biashara au sehemu za biashara zenye anwani sahihi kwa ajili ya kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha.

(2) Kwa kuzingatia kifungu hiki, mtoa huduma ndogo za fedha hataruhusiwa kufungua au kufunga sehemu ya biashara bila kupata idhini ya Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(3) Mtoa huduma ndogo za fedha ambaye atashindwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, atakuwa anatenda kosa.

Uendeshaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha

7.-(1) Taratibu za uendeshaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha zitakuwa kama itakavyoainishwa katika sheria zao anzilishi au katiba zinazoanzisha taasisi husika.

(2) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (1), Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza, iwapo itajiridhisha kuwa utaratibu wa uendeshaji wa taasisi ya huduma ndogo za fedha unakinzana na biashara ya huduma ndogo za fedha,

itatoa maelekezo ya jumla au mahsusi kwa taasisi ya huduma ndogo ya fedha kuhusu uendeshaji wake na maelekezo hayo yatapaswa kutekelezwa.

Uwajibikaji wa watoa huduma ndogo za fedha

8. Mtoa huduma ndogo za fedha atapaswa, kwa dhumuni la kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha, kuwajibika kwa Benki Mamlaka Kasimishwa au mamlaka nyingine yoyote kwa mujibu wa sheria zinazotumika.

Kiwango cha chini cha mtaji

9. Mtoa huduma ndogo za fedha anayefanya biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Sheria hii, atapaswa kutekeleza matakwa ya kuwa na kiwango cha chini cha mtaji kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Kiwango cha chini cha mali zinazobadilis hi-ka kirahisi kuwa fedha taslim

10.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha atapaswa kuwa na kiwango cha chini cha mali zinazobadilishika kirahisi kuwa fedha taslim kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(2) Kwa dhumuni la kifungu hiki, “mali zinazobadilishika kirahisi kuwa fedha taslim” maana yake ni-

(a) noti na sarafu ambazo ni fedha halali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(b) bakaa zilizopo katika benki au taasisi za huduma ndogo ya fedha;
(c) dhamana na hatifungani za Serikali ambazo ni rahisi kuuzika kupitia Benki; au
(d) mali nyingine kama Benki au Mamlaka Kasimishwa itakavyobainisha.

Kuhama madaraja kwa watoa huduma ndogo za fedha

11.-(1) Taasisi yoyote ya huduma ndogo za fedha inaweza, kwa kutuma maombi na kukidhi vigezo vilivyoainishwa katika kanuni, kuhama kutoka Daraja moja la watoa huduma ndogo za fedha kwenda Daraja jingine.

(2) Endapo taasisi ya huduma ndogo za fedha inahama kwenda daraja jingine, taasisi hiyo itapaswa kusimamiwa kwa mujibu wa sheria zinazohusika na daraja husika pamoja na Sheria hii.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, vigezo vya kuhama daraja kwa taasisi ya huduma ndogo za fedha vitajumuisha-

(a) kiwango cha chini cha mtaji kinachokidhi kuhamia daraja husika;

(b) idadi ya wanachama na wateja inayokidhi kuhamia daraja husika;

(c) aina ya shughuli ya huduma ndogo za fedha inayofanywa; na

(d) vigezo vingine vyovyote kama vitakavyoainishwa katika kanuni.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, Benki inaweza, kabla ya kutoa idhini ya kuruhusu taasisi ya huduma ndogo za fedha kuhama kwenda daraja jingine, kufanya tathmini ili kujiridhisha uendelevu wa huduma za taasisi hiyo baada ya kuhamia daraja jingine.

(5) Endapo baada ya kufanya tathmini, Benki itajiridhisha kwamba taasisi ya huduma ndogo za fedha inakidhi vigezo vya kuhama, inaweza kutoa maelekezo ya kuiruhusu taasisi hiyo kuhama kwa kuzingatia vigezo na masharti yatakayotolewa na Benki.

(6) Endapo taasisi ya huduma ndogo za fedha, bila sababu za msingi, itashindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (5), Benki itachukua hatua stahiki ili kuhakikisha maelekezo yake yanatekelezwa.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YANAYOHUSU MASUALA YA UTAWALA

Majukumu ya Benki

12.-(1) Benki itakuwa na jukumu la kusimamia na kufuatilia taasisi za watoa huduma ndogo za fedha zinazofanya biashara ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), majukumu ya Benki yatakuwa ni kudhibiti na kusimamia uendeshaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa Sheria hii na sheria nyingine husika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya vifungu vidogo vya (1) na (2), Benki itakuwa na majukumu yafuatayo-
(a) kutoa leseni kwa watoa huduma ndogo za fedha waliokidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria hii;
(b) kushauri na kutoa taarifa kwa Waziri kuhusu masuala ya biashara ya huduma ndogo za fedha;
(c) kuanzisha na kusimamia kanzidata ya watoa huduma ndogo za fedha;
(d) kukagua, kufuatilia na kutathmini utendaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha;
(e) kutoa nyaraka na miongozo kwa watoa huduma ndogo za fedha;
(f) kutathmini na kutoa idhini kwa watoa huduma ndogo za fedha kuhama daraja moja kwenda jingine;
(g) kuhakikisha malalamiko yanayohusu biashara ya huduma ndogo za fedha yanashughulikiwa ipasavyo;
(h) kuhakikisha ulinzi kwa watumiaji wa huduma ndogo za fedha ikijumuisha kutoa adhabu kwa ukopeshaji usiofuata misingi na taratibu sahihi za ukopeshaji;
(i) kuhakikisha kuwa taarifa za mikopo ya biashara ya huduma ndogo za fedha zinakusanywa, kusambazwa na kupatikana kwa urahisi; na
(j) kutekeleza majukumu mengine kama itakavyotakiwa kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha.

Mamlaka ya Benki

13. Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Benki itakuwa na mamlaka ya-
(a) kuchunguza au kuhoji uendeshaji wa shughuli za watoa huduma ndogo za fedha;
(b) kukagua na kuchunguza vitabu vya hesabu, kumbukumbu, taarifa na nyaraka nyingine yoyote ya watoa huduma ndogo za fedha;
(c) kutaka na kupewa taarifa zinazohusu shughuli za watoa huduma ndogo za fedha;

(d) kuelekeza usimamizi bora wa shughuli za watoa huduma ndogo za fedha;

(e) kuingia, kwa muda wowote muafaka, kwenye eneo lolote la biashara la mtoa huduma ndogo za fedha au eneo lolote ambalo inaaminika, kwa sababu za msingi, kwamba vitabu vya hesabu, kumbukumbu au nyaraka za biashara ya mtoa huduma ndogo za fedha katika namna yoyote zinatunzwa;

(f) kufungua au kuagiza kufunguliwa kwa chumba au kasha la kuhifadhia fedha au kifaa kingine ambapo kunashukiwa, kwa sababu za msingi, kwamba kuna amana, vitabu vya hesabu, kumbukumbu au nyaraka za mtoa huduma ndogo za fedha;

(g) kumuagiza afisa yeyote, mwajiriwa au wakala yeyote wa mtoa huduma ndogo za fedha kutoa au kuwasilisha maelezo au nyaraka zinazohusu usimamizi au shughuli za mtoa huduma ndogo za fedha; na

(h) kutekeleza mamlaka mengine kama itakavyokuwa lazima kwa utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Kukasimisha mamlaka na majukumu ya Benki

14.-(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu na mamlaka yake ya udhibiti na usimamizi chini ya Sheria hii na kwa kuzingatia masharti na taratibu mahsusi ambazo zitawekwa na Benki, Benki inaweza, kwa notisi itakayotangazwa kwenye Gazeti la Serikali, kukasimisha majukumu au mamlaka yake yoyote kama ifuatavyo:

(a) kwa majukumu na mamlaka ya watoa huduma ndogo za fedha waliopo katika Daraja la 3, kwa Tume; na

(b) kwa majukumu na mamlaka ya watoa huduma ndogo za fedha waliopo katika Daraja la 4, kwa mamlaka za serikali za mitaa.

(2) Mamlaka Kasimiwa chini ya kifungu kidogo cha (1), zinapaswa kutekeleza majukumu na mamlaka yake kwa mujibu wa masharti, taratibu na maelekezo mengine yoyote yatakayotolewa na Benki mara kwa mara.

(3) Mamlaka au jukumu lolote lililokasimishwa chini ya kifungu hiki, litakapotekelezwa na Mamlaka Kasimiwa litachukuliwa kama limetekelezwa na Benki.

(4) Ukasimishaji wa mamlaka chini ya kifungu hiki hautazuia Benki kutekeleza mamlaka na majukumu yake yaliyokasimishwa.

(5) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), isipokuwa pale Waziri atakapoidhinisha vinginevyo, Benki haitakuwa na mamlaka ya kukasimisha majukumu na mamlaka yake yanayohusu udhibiti na usimamizi wa taasisi za watoa huduma ndogo za fedha katika Daraja la 2.

Sura ya 287 na 288

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, tafsiri ya neno "mamlaka za serikali za mtaa" ina maana iliyotolewa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji).

Jukumu la Waziri

15.-(1) Waziri atakuwa, kwa madhumuni ya kuhakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya kisera kwa biashara ya huduma ndogo za fedha, na jukumu la kutunga sera na kusimamia utekelezaji wake.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Waziri atatekeleza yafuatayo-

(a) kuweka mazingira wezeshi ya kusaidia ustawi wa biashara ya huduma ndogo za fedha;
(b) kuhakikisha biashara ya huduma ndogo za fedha inakuwa endelevu;
(c) kutoa maelekezo kwa Benki katika utekelezaji wa sera ya biashara ya huduma ndogo za fedha;
(d) kuhakikisha uwepo wa uendelezaji, uwazi na uwajibikaji katika biashara ya huduma ndogo za fedha; na
(e) kutekeleza jukumu jingine lolote kwa utekelezaji bora wa Sheria hii.

(3) Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Mawaziri husika, kuhitaji au kutaka kupatiwa taarifa au nyaraka zinazohusu biashara ya huduma ndogo za fedha kutoka Wizara, taasisi au ofisi yoyote na Wizara, taasisi au ofisi hiyo itapaswa kutekeleza.

(4) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Waziri

mwenye dhamana na ushirika au kadri itakavyokuwa, Waziri mwenye dhamana na mamlaka za serikali za mitaa, kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

SEHEMU YA NNE
UTOAJI LESENI KWA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA WA DARAJA LA 2 NA 3

Katazo la kutoa huduma ndogo za fedha bila leseni

16.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 28 cha Sheria hii, mtu hapaswi kufanya shughuli yoyote ya kutoa huduma ndogo za fedha isipokuwa kama mtu huyo amepatiwa leseni kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia-

(a) kwa Daraja la 2, atapata adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni ishirini na isiyozidi shilingi milioni mia moja au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja;

(b) kwa Daraja la 3, atapata adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni hamsini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

(c) kwa Daraja la 3, atapata adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Maombi ya leseni kwa Daraja la 2

17.-(1) Mtu anayekusudia kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 2 atapaswa kuomba leseni kutoka Benki kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(2) Maombi ya leseni chini ya Daraja la 2 yatapaswa kuwasilishwa Benki kupitia fomu maalum kama zitavyoonyeshwa katika kanuni, na maombi hayo yatapaswa kuwa na taarifa za mwombaji, biashara ya huduma ndogo za

fedha husika, mahala au sehemu ya biashara na taarifa nyingine kama itakavyohitajika kwa madhumuni hayo.

(3) Maombi yatakayowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1), yatapaswa kuambatishwa na-

(a) nakala iliyothibitishwa ya hati ya usajili iliyotolewa kwa mujibu wa sheria husika;

(b) ada ya maombi iliyoainishwa ambayo haitarejeshwa; na

(c) taarifa au nyaraka nyingine kama itakavyohitajiwa na Benki kwa madhumuni ya maombi hayo.

(4) Benki itatengeneza kanuni zitakazoainisha utaratibu wa maombi ya leseni na masuala mengine yanayohusu wakopesshaji binafsi wa fedha.

Maombi ya leseni kwa Daraja la 3

18.-(1) Mtu anayekusudia kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 3 atapaswa kuomba leseni kutoka Benki au Mamlaka Kasimiwa kwa utaratibu utakaowekwa katika kanuni.

(2) Maombi ya leseni chini ya Daraja la 3 yatapaswa kuwasilishwa Benki au kwa Mamlaka Kasimiwa kupitia fomu maalum na maombi hayo yatapaswa kuambatanishwa na-

Sura ya 211

(a) nakala iliyothibitishwa ya hati ya usajili iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika;

(b) ada ya maombi iliyoainishwa ambayo haitarejeshwa; na

(c) taarifa au nyaraka nyingine kama itakavyohitajika na Benki au Mamlaka Kasimiwa kwa madhumuni ya maombi ya leseni.

Utoaji wa leseni kwa mtoa huduma ndogo za fedha wa kigeni

19.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha wa kigeni anayetaka kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha atapaswa kutuma maombi ya leseni kwa Benki.

(2) Utaratibu wa maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) utaainishwa kwenye kanuni.

(3) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha wa kigeni atafanya biashara ya huduma ndogo za fedha nchini, mtoa

huduma ndogo za fedha huyo atapaswa kuzingatia sheria husika za ushirikishwaji wa wazawa ikijumuisha ajira na mafunzo.

Upitiaji wa maombi

20. Baada ya kupokea maombi chini ya Sheria hii, Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza, ndani ya kipindi kitakachoainishwa katika kanuni, kuyafanyia kazi maombi yaliyopokelewa ili kujiridhisha iwapo yamezingatia matakwa ya kisheria yaliyoainishwa.

Utoaji leseni

21. Endapo Benki au Mamlaka Kasimiwa itaridhika kuwa mwombaji amekidhi matakwa yote ya kupewa leseni chini ya Sheria hii, Benki au Mamlaka Kasimiwa itapaswa:

(a) kutoa leseni kwa mwombaji yenye vigezo na masharti kama Benki au Mamlaka Kasimiwa itakavyoona inafaa; na

(b) kusajili mtoa huduma ndogo za fedha aliyepewa leseni katika rejesta.

Uhalali wa leseni

22. Leseni iliyotolewa chini ya Sheria hii itakuwa halali kuanzia tarehe iliyotolewa na itakuwa halali isipokuwa kama itafutwa na Benki au Mamlaka Kasimiwa.

Kukataa maombi ya leseni

23.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kukataa kutoa leseni iwapo-

(a) mwombaji ameshindwa kukidhi vigezo na masharti ya kupata leseni; au

(b) mwombaji ametoa taarifa zisizo sahihi au zinazopotosha.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimiwa itakataa kutoa leseni, itapaswa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya uamuzi wake, kumtaarifu mwombaji kwa maandishi sababu za kukataa.

Maombi mapya na kukata rufaa

24.-(1) Mwombaji ambaye maombi yake yatakataliwa anaweza kuomba upya, iwapo mapungufu yaliyokuwa msingi wa kukataliwa kwa maombi ya awali au mapitio ya maombi yamerekebishwa au vinginevyo yameshughulikiwa.

(2) Mwombaji asiyeridhika na uamuzi ya Benki au Mamlaka Kasimiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) anaweza, ndani ya siku ishirini na moja kuanzia tarahe ya uamuzi-

(a) iwapo ni Mamlaka Kasimiwa, kukata rufaa kwa Benki; au

(b) iwapo ni Benki, kukata rufaa kwa Waziri.

(3) Mtu ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Waziri chini ya kifungu hiki, anaweza kutafuta nafuu kwenye mahakama yenye mamlaka stahiki.

Ufutaji wa leseni

25.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza, kwa kutoa notisi kwa mtoa huduma ndogo za fedha, kufuta leseni pale ambapo mtoa huduma ndogo za fedha-

(a) atasitisha biashara ya huduma ndogo za fedha;

(b) atakiuka vigezo na masharti yaliyowekwa kwenye leseni;

(c) atafilisika au vinginevyo kufutwa;

(d) atafutiwa usajili chini ya sheria husika; au

(e) atakiuka masharti ya Sheria hii.

(2) Benki au Mamlaka Kasimiwa, ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kufutwa leseni, itapaswa kuchapisha jina la mtoa huduma ndogo za fedha aliyefutiwa leseni katika Gazeti la Serikali na gazeti linalosambazwa kwa wingi kwa umma.

Utaratibu wa kufuta leseni

26.-(1) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atakiuka vigezo na masharti ya leseni iliyotolewa, Benki au Mamlaka Kasimiwa itatoa notisi ya maandishi kwa mtoa huduma ndogo za fedha inayobainisha ukiukwaji uliofanyika na muda ambao ukiukwaji huo unapaswa kurekebishwa.

(2) Baada ya mtoa huduma ndogo za fedha kupokea notisi ya ukiukwaji, atapaswa kuwasilisha kwa Benki au Mamlaka Kasimiwa maelezo kuhusu marekebisho ya ukiukwaji au kasoro iliyofanyika .

(3) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa kurekebisha au kusahihisha makosa ndani ya muda ulioainishwa katika notisi au hatawasilisha maelezo yanayojitosheleza, Benki au Mamlaka Kasimiwa itafuta

leseni iliyotolewa na kumtaarifu ipasavyo mtoa huduma ndogo za fedha kwa maandishi.

(4) Mtoa huduma ndogo za fedha ambaye hakuridhika na uamuzi wa Benki au Mamlaka Kasimiwa ya kufuta leseni, anaweza-

(a) iwapo uamuzi ulifanywa na Benki, kukata rufaa kwa Waziri; na

(b) iwapo uamuzi ulifanywa na Mamlaka Kasimiwa, kukata rufaa kwa Benki.

(5) Mtu ambaye hataridhishwa na uamuzi wa Waziri chini ya kifungu hiki, anaweza kutafuta nafuu kwenye mahakama yenye mamlaka stahiki.

Matokeo ya kufuta leseni

27.-(1) Endapo leseni ya mtoa huduma ndogo za fedha itafutwa kwa mujibu wa Sheria hii, Benki au Mamlaka Kasimiwa itapaswa kufuta jina la mtoa huduma ndogo za fedha kutoka kwenye rejesta na kwa maandishi itamwelekeza mtoa huduma ndogo za fedha-

(a) kusimamisha shughuli zake kuanzia tarehe ya kufutwa kwa leseni;

(b) kusimamia na kushughulikia ndani ya muda utakaoainishwa, masuala yote yanayohusu mali na madeni ya watumiaji au wanachama.

(2) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa kutekeleza maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), Benki itakuwa na mamlaka ya kuchukua hatua stahiki kulinda haki za watumiaji au wanachama.

SEHEMU YA TANO
USAJILI WA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA WA DARAJA LA 4

Usajili wa watoa huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 4

28.-(1) Mtu anayekusudia kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 4 atapaswa kuwasilisha Benki au Mamlaka Kasimiwa maombi ya kusajiliwa kwa utaratibu utakaoanishwa katika kanuni.

(2) Maombi ya kusajiliwa yatawasilishwa Benki au katika Mamlaka Kasimiwa kwa kutumia fomu maalum na maombi hayo yatapaswa kuambatanishwa na-

(a) nakala mbili za katiba zilizotiwa saini na wanachama wa mwombaji;
(b) azimio la wanachama la kuanzisha na kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha ambalo limesainiwa na wanachama wote;
(c) muundo wa kikundi unaopendekezwa na majina ya viongozi yanayopendekezwa na mwombaji;
(d) barua ya utambulisho kutoka kwenye kata au serikali ya kijiji inayomtambulisha mwombaji; na
(e) nyaraka au taarifa nyingine zozote ambazo Benki au Mamlaka Kasimiwa zitazihitaji.

Kukataa maombi ya usajili kwa Daraja la 4

29.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 28 cha Sheria hii, Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kukataa kumsajili mwombaji iwapo-
(a) ameshindwa kutimiza vigezo vya usajili; au
(b) ametoa taarifa zisizo sahihi au zinazopotosha.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimiwa imekataa kumsajili mwombaji chini ya kifungu hiki, itapaswa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya uamuzi wake, kumjulisha mwombaji kwa maandishi sababu za kukataa kumsajili.

(3) Mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa kwa mujibu wa kifungu hiki anaweza kuwasilisha maombi mpya kwa kuzingatia sababu za kukataliwa kwa maombi yake na maombi hayo yatashughulikiwa kama maombi mapya na yatafuata taratibu zote za maombi.

(4) Mtu ambaye hataridhishwa na uamuzi chini ya kifungu hiki anaweza-
(a) kwa uamuzi uliyofanywa na Mamlaka Kasimiwa, kata rufaa kwa Benki; na
(b) kwa uamuzi uliyofanywa na Benki, kata rufaa kwa Waziri.

Hati ya usajili

30.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa mara baada ya kufanya usajili wa mtoa huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 4, itatoa kwa mtoa huduma huyo hati ya usajili.

(2) Hati ya usajili inayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) itajumuisha-
(a) jina na anwani ya mtoa huduma ndogo za fedha;

(b) tarehe na uhalali wa usajili;
(c) eneo la shughuli au sehemu ya biashara ya mtoa huduma ndogo za fedha; na
(d) vigezo na masharti mengine yatakayohitajika.

Matokeo ya usajili

31.-(1) Hati ya usajili itakuwa ndiyo ushahidi kwa mtoa huduma ndogo za fedha kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha kwa kuzingatia masharti ya katiba yake na Sheria hii.

(2) Mtoa huduma ndogo za fedha aliyesajiliwa atakuwa na hadhi ya taasisi hodhi na kwa kutumia jina lake itaweza-

(a) kushtaki na kushtakiwa;
(b) kupata, kununua au kwa namna nyingine kuuza mali zinazohamishika au zisizohamishika;
(c) kuingia mkataba; na
(d) kutekeleza mambo yote ambayo yanaweza kufanywa na taasisi hodhi na ambayo ni ya lazima kwa ajili ya utekelezaji wa kazi na majukumu yake.

(3) Mtu au kikundi chochote ambacho kinajihusisha na biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya Daraja la 4 bila kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii anatenda au kinatenda kosa.

Ufutaji hati ya usajili

32.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kufuta hati ya usajili iwapo itajiridhisha kuwa:

(a) vigezo na masharti yaliyowekwa katika hati ya usajili yamekiukwa;
(b) mtoa huduma ndogo za fedha ameacha kutoa huduma; na
(c) mtoa huduma ndogo za fedha anatoa huduma kinyume na masharti ya Sheria hii au sheria nyingine husika.

(2) Endapo hati ya usajili imefutwa, Benki au Mamlaka Kasimiwa itafanya yafuatayo:

(a) kumfahamisha mtoa huduma ndogo za fedha kwa maandishi sababu za kufutwa kwa usajili;
(b) kumwagiza mtoa huduma ndogo za fedha kusitisha shughuli zake; na

(c) kufuta jina la mtoa huduma ndogo za fedha huyo katika rejesta.

(3) Masharti ya kifungu cha 26 cha Sheria hii kuhusu taratibu za kufuta leseni yatatumika kwa kuweka marekebisho madogo stahiki katika kufuta hati ya usajili iliyotolewa chini ya Sheria hii.

Uendelezaji na uwezeshaji watoa huduma ndogo za fedha

33.-(1) Kwa madhumuni ya kuendeleza ukuaji na uendelevu wa mtoa huduma ndogo za fedha katika Daraja la 4, Benki kwa kushirikiana na Baraza-

(a) itatoa elimu ya masuala ya fedha kwa wanachama wa watoa huduma ndogo za fedha;
(b) itaendeleza na kuingilia kati iwapo italazimika kwa kuwaendeleza watoa huduma ndogo za fedha;
(c) italinda maslahi na haki za wanachama na wanufaika wa watoa huduma ndogo za fedha;
(d) itatoa msaada kwa mtoa huduma ndogo za fedha kupitia programu mbalimbali za Serikali;
(e) itafanya kazi nyingine kwa madhumuni ya kuendeleza na kuwawezesha watoa huduma ndogo za fedha.

(2) Katika kifungu hiki "Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lililoanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI NA UDHIBITI WA WATOA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA
(a) Usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha

Usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha

34. Usimamizi wa shughuli, masuala ya fedha na biashara ya huduma ndogo za fedha utafanywa na mtoa huduma ndogo za fedha.

Usimamizi na utwaaji

35.-(1) Bila ya kujali kifungu cha 34 na sheria nyingine husika, Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza

kutwaa usimamizi wa huduma ndogo ya fedha endapo-

(a) Benki au Mamlaka Kasimiwa inaona kuwa mtoa huduma ndogo za fedha-
  (i) hana uwezo wa kifedha;
  (ii) hafanyi kazi zake kwa mujibu wa taratibu bora za kiutawala na kihasibu; na
  (iii) hazingatii sera sahihi za udhibiti wa viashiria vya hatari;

(b) mtoa huduma ndogo za fedha ameshindwa kuzingatia masharti ya kiwango cha chini cha mtaji yaliyoainishwa na Sheria hii;

(c) mtoa huduma ndogo za fedha anakataa kukaguliwa na Benki au Mamlaka Kasimiwa kama inavyotakiwa na Sheria hii;

(d) leseni ya mtoa huduma ndogo za fedha imefutwa;

(e) kuendelea kwa biashara hiyo ya huduma ndogo za fedha kutaathiri maslahi ya mteja wa huduma ndogo za fedha; au

(f) mtoa huduma ndogo za fedha anafanya biashara ya huduma ndogo za fedha kinyume na Sheria hii.

(2) Mdaawa katika mkataba na mtoa huduma ndogo za fedha hataondolewa wajibu wake kwa kigezo kwamba mtoa huduma ndogo za fedha yupo chini ya usimamizi ya Benki au Mamlaka Kasimiwa.

(3) Gharama za usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha wakati wa kipindi cha kutwaliwa hazitabebwa na Benki au Mamlaka Kasimiwa.

(4) Utaratibu wa usimamizi na utwaaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha chini ya kifungu hiki utakuwa kama utakavyoainishwa katika kanuni.

Shughuli zinazozuiliwa na zinazokubalika

36.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha hatajihusisha na kutoa huduma yoyote iliyozuiliwa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote ya Bunge.

(2) Benki, kupitia kanuni, itaainisha shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa kwa watoa huduma ndogo za fedha.

(3) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa, bila sababu ya msingi, kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itapaswa kuchukua hatua stahiki kama itakavyofaa kuhakikisha masharti yanazingatiwa.

Ulipaji wa gawio au riba

37.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha atapaswa kuwalipa wanahisa wake gawio au atafanya utaratibu mwingine wowote wa mgao au kuwalipa riba wanahisa au wanachama wake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na sheria nyingine husika.

(2) Malipo ya gawio, riba na aina yoyote ya mgao chini ya kifungu kidogo cha (1), ikijumuisha kipindi cha malipo, itakuwa kwa namna itakavyoainishwa kwenye katiba au kwenye nyaraka nyingine husika za mtoa huduma ndogo za fedha.

Vitabu vya mahesabu na kumbukumbu nyinginezo

38. Mtoa huduma ndogo za fedha atatunza vitabu sahihi vya mahesabu pamoja na kumbukumbu nyingine zinazohusiana na biashara yake ambazo zinatosheleza, kuonyesha na kuelezea miamala aliyoifanya pamoja na masuala ya kifedha.

Uandaaji wa mahesabu

39.-(1) Kila mtoa huduma ndogo za fedha kwa kila mwaka wa fedha atapaswa kuandaa mahesabu katika viwango vilivyoainishwa.

(2) Viwango vilivyoainishwa kwa ajili ya kuandaa mahesabu ya biashara ya watoa huduma ndogo za fedha vitazingatia vigezo vya kitaifa vya utayarishaji wa taarifa za fedha.

(3) Hesabu na taarifa nyingine za fedha za biashara ya huduma ndogo za fedha zitawasilishwa kwa kutumia shilingi ya Kitanzania na zitazingatia matakwa ya sheria husika.

Ukaguzi wa mahesabu

40.-(1) Hesabu za biashara ya huduma ndogo za fedha, isipokuwa kwa mtoa huduma ndogo za fedha wa Daraja la 4, zitakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na mkaguzi kwa namna ilitakavyoainishwa kwenye kanuni.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha

(1), hesabu na taarifa nyingine za fedha za watoa huduma ndogo za fedha kwa Daraja la 4 zitakaguliwa au kufuatiliwa kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Kasimiwa itajiridhisha kwamba hesabu zilizokaguliwa za mtoa huduma ndogo za fedha hazijakidhi masharti ya Sheria hii au kanuni husika au zimejumuisha taarifa inayoweza kupotosha au iwapo hazijatangazwa kwa utaratibu ulioainishwa katika fomu, Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kumtaka mtoa huduma-

(a) kuzifanyia marekebisho hesabu hizo zilizokaguliwa ili kutimiza matakwa ya Sheria;
(b) kurekebisha taarifa zinazopotosha;
(c) kuchapisha upya hesabu zilizorekebishwa; na
(d) kuwasilisha kwa Benki au kwa Mamlaka Kasimiwa nyaraka au taarifa za ziada zinazohusiana na nyaraka au taarifa yoyote.

(4) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha, bila sababu ya msingi, atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Uteuzi wa mkaguzi wa ndani

41.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha atateua mkaguzi wa hesabu wa ndani ambaye atakuwa na elimu na uzoefu ulioanishwa kwenye kanuni husika.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), mtoa huduma ndogo za fedha kwa Daraja la 4 atateua mtu atakayekuwa na dhamana ya usimamizi wa ndani wa masuala ya fedha ya mtoa huduma huyo kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Utoaji wa taarifa za fedha

42.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha atatoa taarifa zake za fedha kwa Benki, Mamlaka Kasimiwa na wadau wengine kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), mtoa huduma ndogo za fedha, kwa kipindi chote cha mwaka na katika sehemu ya biashara inayoonekana, ataweka nakala ya hesabu za fedha zilizokaguliwa kwa kipindi husika, nakala ya mizania ya hesabu na akaunti ya faida na hasara kwa

muundo na namna itakavyoainishwa na Benki au Mamlaka Kasimiwa.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kuainisha namna ambavyo mtoa huduma ndogo za fedha wa Daraja la 4 atakavyotoa taarifa zake za fedha.

(4) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha, bila sababu za msingi, atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyofaa ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Utoaji wa taarifa za mikopo

43.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha atatoa taarifa za mikopo kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, taarifa za mikopo zitajumuisha taarifa zozote zikiwemo taarifa binafsi na historia ya mikopo ya mkopaji kama vile mwenendo wa urejeshaji wa mikopo, madeni ambayo hayajalipwa, madeni ya kodi na taarifa nyingine zozote za kibiashara.

(3) Bila ya kujali vifungu vidogo vya (1) na (2), kwa madhumuni ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa za mikopo, kila mtoa huduma ndogo za fedha wa Daraja la 2, 3 na 4 atatoa taarifa za mikopo kwa chombo cha ubadilishaji taarifa za mikopo

(4) Mtoa huduma ndogo za fedha anaweza kupata na kutumia taarifa za mikopo kupitia chombo cha ubadilishanaji taarifa za mikopo kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Sura 197

(5) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, udhibiti wa taarifa za mikopo utafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Benki.

(6) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa, bila sababu za msingi, kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua stahiki ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

(b) Usimamizi wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha

Uwasilishaji wa taarifa

44.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha atawasilisha kwa Benki au kwa Mamlaka Kasimiwa taarifa za biashara

yake ya huduma ndogo za fedha kwa kipindi na kwa namna itakavyoainishwa katika Benki.

(2) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha, bila sababu za msingi, atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Upatikanaji wa taarifa za muda

45.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa itakuwa na mamlaka ya kupata taarifa zinazohusu shughuli za watoa ya huduma ndogo za fedha wowote na inaweza kuelekeza, kwa maandishi, kwamba taarifa hiyo iwasilishwe ndani ya muda ulioanishwa kwenye maelekezo.

(2) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha, bila sababu za msingi, atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Usiri

46.-(1) Endapo Benki au Mamlaka Kasimiwa au mtoa huduma ndogo za fedha atakuwa na taarifa iliyopatikana chini ya Sheria hii, taarifa hiyo itaichukuliwa kuwa ni siri na haitatolewa kwa mtu yeyote.

(2) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (1), Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kutoa taarifa yoyote-

(a) kwa mtu au taasisi iliyoidhinishwa endapo taarifa hiyo inahitajika na ni kwa ajili ya usimamizi au udhibiti na usiri wake utaendelea kulindwa; au

(b) kwa mujibu wa sheria, amri ya mahakama au kwa ridhaa ya mtumiaji wa huduma ndogo za fedha husika.

Ukaguzi wa biashara ya huduma ndogo za fedha

47.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza, kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni, kukagua mtoa huduma ndogo za fedha yeyote.

(2) Itakuwa ni wajibu wa mtoa huduma ndogo za fedha kumwonyesha afisa yeyote aliyeruhusiwa kufanya ukaguzi, vitabu vyote vya hesabu, kumbukumbu na nyaraka nyingine zilizo chini ya mamlaka au uangalizi wa mtu huyo

na kutoa maelezo au taarifa yoyote inayohusu na shughuli za mtoa huduma ndogo za fedha kama ambavyo mamlaka ya ukaguzi itakavyohitaji katika muda utakaoainishwa.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Kasimiwa, baada ya kuzingatia ripoti ya ukaguzi chini ya kifungu kidogo cha (1), itabaini kwamba shughuli za mtoa huduma ndogo za fedha zinawaathiri wateja wake au zinafanywa kinyume na Sheria hii, inaweza, baada ya kumpa mtoa huduma ndogo za fedha haki ya kujieleza kuhusiana na ripoti hiyo, kuchukua hatua kwa namna itakavyoona inafaa, ikijumuisha-

(a) kumzuia, kumsitisha au kumkataza mtoa huduma ndogo za fedha kulipa gawio;

(b) kusitisha leseni kwa kipindi ambacho Benki au Mamlaka Kasimiwa itaona inafaa;

(c) kuzuia uhamishaji wa faida yoyote ya mtoa huduma ndogo za fedha kwenda kwenye mtaji;

(d) kumwelekeza mtoa huduma ndogo za fedha kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya afisa yeyote aliyehusika na kitendo hicho;

(e) kumwelekeza mtoa huduma ndogo za fedha kuunda upya menejimenti yake;

(f) kumwelekeza mtoa huduma ndogo za fedha, ndani ya muda ulioainishwa, kuwasilisha Benki au kwa Mamlaka Kasimiwa-

(i) mpango wa urejeshaji wa mtaji; au

(ii) mpango wa kurekebisha mapungufu yote kwa namna ambavyo Benki au Mamlaka Kasimiwa itajiridhisha;

(g) kumzuia mtoa huduma ndogo za fedha asitoe bonasi, nyongeza ya mshahara na marupurupu mengine kwa uongozi wa juu wa menejimenti au kwa maafisa wa watoa huduma ndogo za fedha;

(h) kuzuia ongezeko la mali au madeni ya huduma ndogo za fedha kwa namna itakavyoona inafaa;

(i) kumtaka mtoa huduma ndogo za fedha kufanya au kuchukua hatua nyingine yoyote kama ambavyo Benki au Mamlaka Kasimiwa itakavyoona inafaa.

(4) Mtu yeyote atakayemzuia afisa wa Benki au wa Mamlaka Kasimiwa au mtu mwingine yeyote

aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu yake chini ya kifungu hiki, au ambaye anapuuza au kukataa kuonyesha vitabu, kumbukumbu au kitu chochote ambacho afisa wa Benki au wa Mamlaka Kasimiwa au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa atakapohitaji kupatiwa kwa ajili ya ukaguzi, atakuwa ametenda kosa.

Usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha kwa Daraja la 4

48.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa itafanya au kuagiza kufanyika usimamizi endelevu wa biashara na shughuli za mtoa huduma ndogo za fedha wa Daraja la 4 kwa mujibu wa kanuni husika.

(2) Endapo baada ya kufanya usimamizi chini ya kifungu kidogo cha (1), Benki au Mamlaka Kasimiwa itabaini mapungufu kwenye usimamizi wa biashara ya huduma ndogo za fedha, Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza-

(a) kushauri au kumwelekeza mtoa huduma ndogo za fedha kurekebisha mapungufu ndani ya muda ulioainishwa; au

(b) kumwelekeza mtoa huduma ndogo za fedha kuchukua hatua nyingine zozote ili kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria hii yanatekelezwa.

(3) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa, bila sababu za msingi, kutekeleza amri au maelekezo yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2), Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua stahiki kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha masharti yanatekelezwa.

Uzingatiaji wa Sura ya 423

49.-(1) Mtoa huduma ndogo za fedha ataweka, ili kutekeleza Sheria za Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu, utaratibu wa udhibiti wa ndani kwa lengo la utambuzi wa wateja na kutoa taarifa ya miamala inayotia shaka.

(2) Benki au Mamlaka Kasimiwa itahakikisha kuwa kila mtoa huduma ndogo za fedha anatoa huduma kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1).

SEHEMU YA SABA
ULINZI WA WATUMIAJI WA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Misingi ya kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha

50.-(1) Watoa huduma ndogo za fedha wanapaswa kufuata misingi ya ulinzi wa walaji kwa mujibu wa sheria zinazotumika na katika kanuni zilizotengenezwa chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), misingi ya ulinzi wa walaji wa huduma ndogo za fedha itakayoainishwa katika kanuni, itajumuisha-

(a) vigezo na masharti ya mikopo au huduma zinazohusiana na hizo kuwa ya wazi, usawa, yanayosomeka na yanayolinda haki na maslahi ya watumiaji wa huduma ndogo za fedha au wanachama;
(b) ushughulikiaji wa malalamiko na njia za utatuzi wa migogoro;
(c) utoaji wa taarifa zote husika zinazohusu bidhaa na huduma zinazotolewa;
(d) sharti la kuhakiki masharti ya viwango vya mikataba ya mikopo au makubaliano;
(e) utoaji wa elimu ya fedha kwa wateja;
(f) uwazi katika viwango vya riba, tozo au adhabu; na
(g) misingi mingine yoyote kwa lengo la kuhakikisha usawa kwa watumiaji wa huduma ndogo za fedha.

(3) Kwa mujibu wa kifungu hiki-

"ulinzi kwa mtumiaji" inajumuisha misingi iliyokusudiwa kuhakikisha uwazi wa bidhaa na huduma zinazotolewa na watoa huduma ndogo za fedha, usawa na ulinzi wa maslahi na haki za mtumiaji pamoja na ushughulikiaji wa haki wa malalamiko na njia za utatuzi wa migogoro.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3), kigezo au sharti lolote litakalowekwa katika mkataba au nyaraka husika yoyote zinazodai kumpa mtoa huduma ndogo za fedha mamlaka ya kuweka au kubadilisha kiwango cha riba au masharti mengine yeyote ya mkopo litakuwa ni batili na halitatambulika kisheria.

(5) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa, bila sababu ya msingi, kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua itakayoona inafaa ili kuhakikisha utekelezaji wa masharti yaliyowekwa.

Ukusanyaji wa madeni na fidia

51.-(1) Deni linalotokana na shughuli za biashara za huduma ndogo za fedha chini ya Sheria hii litakusanywa au litafidiwa kwa utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo (1), kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu hiki zitahakikisha-

(a) hatua za ukusanyaji wa deni inaanzishwa kwa kutoa notisi inayojitosheleza ya maandishi kwa mdaiwa;

(b) ukamataji wa mali ya mdaiwa au mali iliyowekwa dhamana kwa ajili ya kuuza ili kufidia deni utafanywa kama njia ya mwisho kabisa; na

(c) muda wa kutosha unaainishwa kama notisi kwa mdaiwa kabla ya kuuza au kuchukua mali ya mdaiwa iliyowekwa dhamana.

(3) Endapo mtoa huduma ndogo za fedha atashindwa, bila sababu ya msingi, kufuata masharti ya kifungu hiki, Benki au Mamlaka Kasimiwa itachukua hatua itakayoona inafaa ili kuhakikisha utekelezaji wa masharti yaliyowekwa.

SEHEMU YA NANE
MAKOSA NA ADHABU

Adhabu ya ujumla

52. Mtu atakayekiuka masharti ya vifungu vya Sheria hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyowekwa, atakuwa ametenda kosa-

(a) kwa Darala la 2 na 3, atahukumiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja; na

(b) kwa Daraja la 4, atahukumiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi

shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Ufililishaji wa makosa

53.-(1) Bila ya kujali vifungu vya Sheria hii vinavyohusu adhabu, iwapo mtu anakubali kwa maandishi kwamba ametenda kosa chini ya Sheria hii, Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza, kwa wakati wowote kabla ya kuanza kusikilizwa na mahakama yenye mamlaka, kuamuru mtu huyo kulipa faini ya papo kwa papo ya kiasi cha fedha kisichozidi nusu ya kiasi cha adhabu ambayo mtu huyo angeweza kuadhibiwa kukilipa kama angehukumiwa kwa kosa hilo.

(2) Endapo kosa limefililishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) na shtaka la kosa limeletwa dhidi ya mtuhumiwa kwa kosa hilo hilo, itakuwa ni ushahidi wa kutosha kwa mtuhumiwa kuithibitishia mahakama katika kiwango cha kuridhisha kuwa kosa analoshitakiwa nalo tayari lilishafililishwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Endapo mtu yeyote hataridhishwa na uamuzi uliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), anaweza, ndani ya muda ulioainishwa, kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo katika Mahakama Kuu na masharti ya vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vitatumika kwenye kila rufaa kana kwamba rufaa hiyo ni dhidi ya uamuzi uliyotolewa na Mahakama ya Wilaya katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

(4) Endapo mtu ameshindwa kutekeleza uamuzi uliyotolewa chini ya kifungu hiki ndani ya muda uliyowekwa, Benki au Mamlaka Kasimiwa:

(a) itamtaka, pamoja na kiasi kilichoamriwa, mtu huyo kulipa riba katika kiwango kitakachoainishwa katika kanuni; na

(b) inaweza kutekeleza amri kwa namna ile ile ya amri ya mahakama katika kulipa kiasi kilichoamriwa katika amri hiyo.

Tangazo la Serikali Na. 711 (Linaendelea.)

SURA YA TISA
MASHARTI YA JUMLA

Daftari la watoa huduma ndogo za fedha

54.-(1) Benki au Mamlaka Kasimiwa itaagiza kuanzishwa kwa Rejesta ya kumbukumbu ya watoa huduma ndogo za fedha wote waliopewa leseni au waliosajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Rejesta hiyo itajumuisha:

(a) jina na anwani ya mtoa huduma ndogo za fedha;

(b) maelezo ya leseni au usajili ikijumuisha tarehe ya leseni na nambe ya cheti kilichotolewa; na

(c) taarifa nyingine kama itakavyoelekezwa na Benki.

(3) Benki au Mamlaka Kasimiwa inaweza kufanya marekebisho yanayohusiana na mabadiliko ya maelezo yoyote ya mtoa huduma ndogo za fedha aliyesajiliwa.

Utangazaji wa watoa huduma ndogo za fedha

55. Benki itapaswa, kwa madhumuni ya uwazi na kuendeleza uelewa kwa umma, kila baada ya miezi sita au katika vipindi ambavyo Benki itaamua, itachapisha katika Gazeti la Serikali na katika gazeti lolote lenye mzunguko mkubwa, majina na anwani kamili za watoa huduma ndogo za fedha-

(a) waliopewa leseni au kusajiliwa kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha;

(b) ambao leseni au hati zao za usajili zimefutwa; na

(c) ambao kwa sababu yoyote ile wameacha kufanya biashara.

Kinga kwa matendo yaliyofanywa au kutekelezwa kwa nia njema
Sura ya 16
Sura ya 17

56. Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 284A cha Sheria ya Kanuni za Adhabu na kifungu cha 3 cha Sheria ya Maafisa wa Umma (Urejeshaji wa Mikopo), hakuna tendo au shughuli itakayofanywa na afisa au wakala wa Benki au Mamlaka Kasimiwa katika kutekeleza au kudaiwa kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria hii, itamwingiza afisa huyo katika hatua, wajibu au madai yoyote.

Masharti ya mpito

57. Mtu ambaye, kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, alikuwa anafanya biashara ya huduma ndogo za

fedha atawajibika ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, kuomba leseni au usajili kwa mujibu wa Sheria hii.

Ushirikishwaji wa wazawa

58. Endapo mtoa huduma ndogo za fedha anafanya biashara ya huduma ndogo za fedha, mtoa huduma huyo atawajibika kufuata na kuzingatia sheria zinazotumika katika kutoa kipaumbele kwa wazawa ikijumuisha ajira na mafunzo kwa Watanzania.

Dhima kwa matendo ya vikundi vya watu

59. Endapo kosa limetendwa chini ya Sheria hii na kikundi cha watu, ama kimesajiliwa au hakikusajiliwa na kikundi hicho kimetenda kosa kwa kufahamu au kushiriki au kuhusishwa na tendo au kosa lolote kwa upande wa mtu au watu wowote ambao wanahusishwa na usimamizi wa kikundi cha watu hao, mtu au watu hao watachukuliwa kuwa wametenda kosa.

Kanuni

60.-(1) Benki inaweza kutengeneza kanuni za jumla kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kutunga kanuni zinazoainisha-

(a) taratibu za maombi na fomu za kuanzisha, kusajili, na kuendesha huduma ndogo za fedha kwa Daraja la 2 na Daraja la 3;
(b) matakwa na taratibu za uanzishaji, usajili na uendeshaji wa watoa huduma ndogo za fedha kwa Daraja la 4;
(c) mambo ambayo yatasimamia shughuli za watoa huduma ndogo za fedha wa Daraja la 4;
(d) masuala ya ukaguzi ikijumuisha uteuzi wa wakaguzi au maafisa waidhiniwa wa mamlaka ya kufanya ukaguzi;
(e) ada mbalimbali zinazolipwa chini ya Sheria hii;
(f) misingi ya kumlinda mtumiaji ikijumuisha taratibu za utatuzi wa migogoro na utoaji wa elimu ya fedha;
(g) namna ambayo elimu ya fedha itatolewa na watoa huduma ndogo za fedha;

(h) malipo yatakayofanywa na masharti ya kuzingatiwa na wanachama au wateja wanaoomba mikopo;
(i) masharti na namna ambayo gawio au aina nyingine za faida zitakavyogawanywa kwa wanachama au wateja;
(j) uteuzi na sifa za mkaguzi wa ndani au mtu aliyeidhinishwa na mtoa huduma ndogo za fedha;
(k) shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa kufanywa na mtoa huduma ndogo za fedha;
(l) uwasilishaji, ukusanyaji na ubadilishanaji wa taarifa ikijumuisha taarifa za mikopo;
(m) vigezo na taratibu za kuhama daraja kwa watoa huduma ndogo za fedha;
(n) hatua mbalimbali za kiutawala kwa kukiuka masharti ya vifungu vya Sheria hii;
(o) masuala yanayohusu biashara ya huduma ndogo za bidhaa zinazofanywa chini ya Sheria hii;
(p) taratibu za uombaji wa leseni na masuala yanayohusu wakopeshaji binafsi wa fedha;
(q) masharti na namna ya uendesdhaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha kimtandao; na
(r) suala lolote ambalo linaweza, au linahitaji kuainishwa na Benki chini ya Sheria hii.

(3) Kanuni zitakazotayarishwa chini ya kifungu hiki zitachapishwa katika Gazeti la Serikali.

Kutotumika kwa baadhi ya masharti kwa Daraja la 4

61. Masharti ya vifungu vya 6(2), 9, 10, 35, 39, 44 na 47 hayatatumika kwa Daraja la 4.

SURA YA KUMI
MAREKEBISHO YATOKANAYO

Vifungu vimeondolewa

62.-68. Vifungu vimeondolewa.